Sasisho la COVID-19 ya Jiji la Burlington

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington (RRC)

Aprili 2021

Kiswahili

Maangazio:

- Ustahiki mpya wa chanjo wa Watu Weusi, Asili na watu wenye rangi katika Vermont
- Mswada wa Msaada wa COVID-19 na Maana Yake
- Ukuaji Mpya wa Kisa cha COVID-19
- Matangazo ya Jimbo
- Mahali pa Kupata Taarifa ya COVID-19
- Jinsi ya kujisajili kwa chanjo

Ustahiki wa Chanjo Umefunguliwa kwa Wakazi WOTE wa Vermont ambao ni Weusi, Asili, au Mtu wa Rangi

Mnamo Machi 30, Jimbo lilitangaza kuwa lingebadilisha ustahiki wa chanjo. Ikiwa wewe au mtu yeyote katika kaya yako anajitambua kama Mweusi, Asili, au mtu wa rangi (BIPOC), watu wote wa kaya walio na umri wa miaka 16 na zaidi wanaweza pia kujisajili ili kupata chanjo. Watu wanaweza kujisajili mtandaoni, kwa kupigia Idara ya Afya, kujisajili kupitia famasia inayoshiriki au kufanya miadi katika kliniki inayolenga BIPOC.

Chaguo za Usajili na Msaada wa Lugha:

1. Jisajili na Idara ya Afya ya Vermont kwenye mtandao katika https://www.healthvermont.gov/covid-19/vaccine/getting-covid-19-vaccine (usajili wa mtandaoni unapatikana katika Kiingereza pekee) au kwa kupiga nambari ya simu ya chanjo katika 855-722-7878 (Kwa usaidizi katika lugha nyingine bonyeza 1). Saa za Kituo cha Simu ni Jumatatu-Ijumaa, 2:15 asubuhi hadi 11:30 jioni na Jumamosi na Jumapili, saa 4:00 asubuhi hadi 9:00 mchana. Tafadhali onyesha lugha unayopendelea ili waweze kuratibu mkalimani awepo wakati wa miadi yako, sawa na kutoa fomu zilizotafsiriwa.

2. Ikiwa una maswali ya ustahiki au unahitaji usaidizi wa usajili katika lugha nyingine, unaweza kuwasiliana na meneja wa kesi yako katika Muungano wa Waafrika au Mpango wa Wakimbizi. Ikiwa huna msimamizi wa kesi, piga simukwa Mpango wa Wakimbizi kupitia 802-655-1963 au Shirika la Waafrika kupitia 802-355-0795 na utaunganishwa na mtu anayezungumza lugha yako. Wanapangisha kliniki yenye wakalimani na usaidizi wa lugha wa ziada.

3. Kliniki zaidi inayolenga BIPOC inapatikana katika Burlington, kupitia ushirikiano wa mashirika kama vile Muungano wa Haki ya Asili katika Vermont, Muungano wa Wataalamu wa Rangi katika Vermont, Mpango wa LEND katika Vermont na Jiji la Burlington. Unaweza kupiga 802-755-7239 ili kuongezwa kwenye orodha ya kusubiri, huduma za mkalimani kwa simu zinatolewa ikiwa utaonyesha lugha unayopendelea. Ukiacha barua ya sauti, tafadhali acha jina lako na lugha unayopendelea na mtu atakupigia kukujibu. Fomu ya usajili wa kwenye mtandao pia inapatikana katika Kiingereza. Tembelea https://bitly.com/BIPOC-Clinics. Tafadhali onyesha lugha unayopendelea ili waweze kuratibu mkalimani awepo wakati wa miadi yako na kutoa fomu zilizotafsiriwa.

Mswada wa Msaada wa Kifedha wa COVID-19

Mswada mpya wa msaada wa kifedha unaoitwa Mpango wa Msaada wa Marekani na Bunge la Marekani mnamo mapema Machi, utakaotoa dola za Marekani trilioni 1.9 katika msaada wa kifedha kwa watu Marekani katika mwaka ujao. Mswada huo unasaidia ufadhili wa mipango ya lishe na maslahi (kama vile usaidizi wa chakula katika Jimbo au mipango ya utunzaji wa watoto), unaendeleza malipo ya watu wasio na ajira, unatoa manufaa ya ushuru, unaunda msaada wa kifedha kwa biashara ndogondogo, na kupatia familia zilizo na watoto na wafanyakazi wasio na watoto msaada wa kifedha wa dharura. Mswada huo pia unapunguza gharama za bima kwa familia zenye mapato ya chini na kati, na kufadhili mipango ya usaidizi wa kodi ya nyumba na bili ya matumizi za siku zijazo. Huku manufaa mengine ni ya mara moja zaidi, mengine yanaweza kuchukua muda kusanidi, tarajia kuona nafasi za msaada wa kifedha zikiendelea kufunguka.

Ukuaji Mpya wa Kisa



Jiji linaendelea kufuatilia uwepo wa **COVID-19 katika jumuiya. Ripoti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kuna ongezeko la visa katika eneo letu, kufikia mwisho wa Machi.** Picha ya hapo juu inaonyesha visa vinavyoongezeka vya COVID-19 katika Kaunti ya Chittenden. Tunagundua kuwa ongezeko la visa sasa linakuwa kawaida zaidi katika vizazi vya watu wadogo, **umri wa wastani wa mtu anayepatikana na maambukizo sasa upo chini ya miaka 30**.Visa vya COVID-19 vinavyohusiana na watu wazee katika jumuiya vinapungua kwa sababu wengi wanachukua fursa ya chanjo.Taarifa hii si ya kuleta kiwewe, lakini ni tahadhari kwa jumuiya kama onyo zaidi.

<u>Unachoweza kufanya:</u>Kwa sababu ya kiwango cha sasa cha visa vya COVID-19 katika Jiji, tafadhali endelea kuvaa barakoa, fuata mwongozo wa Jimbo kuhusu kukusanyika na watu wasio wa kaya yako, na kuzingatia kipimo cha bila malipo (ambacho ni sampuli ya pua lako kwa njia rahisi na kujifanyia, si kipimo cha awali kilichoenda zaidi katika nyuma ya pua lako) kinachopatikana katika 405 Pine Street katika Burlington kila siku kati ya saa 4:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Kupata chanjo pia kunaweza kupunguza kwa kikubwa msambao wa virusi ndani ya jumuiya.

Matangazo ya Jimbo

Katika mwezi uliopita, Jimbo limeweka matangazo kadhaa muhimu:

Mikutano
Kwa watu kaya ambao hawajapata chanjo, mikutano ya watu ndani na nje ya nyumba kikomo cha kaya au watu WAWILI ambao hawajapewa chanjo kwa wakati mmoja, PAMOJA NA kaya yoyote iliyopewa chanjo kamili. Waliopewa chanjo kamili inafafanuliwa kama kila mtu katika kaya amekamilisha dozi zote za chanjo ya COVID-19 zinazohitajika.

Ustahiki wa Umri
Jimbo limetangaza ustahiki wa kikundi cha umri katika siku zijazo, na wakazi wote wa Vermont wenye umri wa miaka 16 na zaidi watakuwa na ustahiki kufika mwishoni wa Aprili.
Umri wa 40+ - Wanaweza kujisajili
Umri wa 30+ - Usajili utafunguliwa Aprili 12
Umri wa 16+ - Usajili utafunguliwa Aprili 19

Ili kuona mwongozo wa Jimbo katika Kiingereza, tembelea:
https://accd.vermont.gov/news/update-new-work-safe-additions-be-smart-stay-safe-order

Mahali pa Kupata Taarifa ya COVID-19

Idara ya Afya ya Vermont sasa ina kurasa za lugha maalum zenye maelezo ya afya ya COVID-19:

Kiarabu: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Arabic
Kifaransa: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#French
Kirundi: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Kirundi
Kinepali:https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Nepali
Kisomali: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Somali
Kiswahili: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Swahili
Kivietnamu: https://www.healthvermont.gov/covid-19/resources/multilingual-resources#Vietnamese

Jopo Kazi la Lugha Anuwai katika Vermont linaendelea kutoa video zilizo na visasisho muhimu. Orodha ya video kwa lugha zinapatikana:

Tembelea ukurasa wao wa wavuti:
https://www.youtube.com/channel/UC3zjPpeFnXqvESr1y3d4DvQ/playlists

Maswali? Je, Unahitaji Usaidizi?

Kituo cha **Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington (RRC)** kiko hapa kukusaidia, wasiliana nasi kupitia 802-755-7239 au recovery@burlingtonvt.gov na uache ujumbe wenye jina lako, lugha unayopendelea, na maelezo ya mawasiliano na tutakusaidia haraka iwezekanavyo. Kituo chetu cha kupokea simu kina huduma za ukalimani kwa simu. Saa zetu za kufanya kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, 2:00 asubuhi hadi 10:30 jioni.

Pata Tafsiri:

Idara ya Afya ya Vermont
https://www.healthvermont.gov/media/translation/covid-19-translations
Jiji la Burlington
https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/translated
Jopo Kazi la Lugha Anuwai katika Vermont:
https://www.youtube.com/channel/UC3zjPpeFnXqvESr1y3d4DvQ

Taarifa katika waraka huu inaweza kubadilika jinsi miongozo inasasishwa katika kiwango cha kitaifa na jimbo